

**TANGAZO LA SERIKARI NA. 119 la tarehe 25/04/2014**

**SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA  
(SURA 287)**

---

**SHERIA NDOGO**

---

**Zimetungwa chini ya kifungu cha 153**

---

**SHERIA NDOGO (UANZISHAJI WA BODI YA MFUKO WA ELIMU)  
ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MUHEZA, 2012**

Jina na tarehe  
ya kutumia

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Uzalishaji wa Bodi ya Mfuko wa Elimu za Halmashauri ya Wilaya ya Muheza za mwaka 2012, na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Muheza.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa kama itatamkwa vinginevyo:-  
“Afisa Elimu wa Halmashauri” maana yake ni mtumishi wa Umma ambaye ndiye msimamizi Mkuu wa utoaji wa huduma za elimu katika Halmashauri ya Wilaya ya Muheza.

“Bodi” maana yake ni Bodi ya Mfuko wa Elimu ya Halmashauri ya Wilaya iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 4 (1) cha sheria ndogo hizi;

“Halmashauri” maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Muheza.

“Kamati ya huduma za jamii ya Halmashauri” maana yake ni kamati ambayo imeanzishwa na Halmashauri kwa mujibu wa sheria ya serikali za mitaa (Mamlaka za Wilaya).

“Kamati ya Utendaji ya mfuko wa Elimu” maana yake ni kamati iliyoteuliwa kwa mujibu wa kifungu cha 30 cha sheria ndogo hizi;

“Katibu mtendaji ” maana yake ni mtendaji Mkuu wa mfuko wa

Elimu wa Halmashauri aliyejiriwa na Bodi ya mfuko wa Elimu kwa mujibu wa kifungu cha 22 cha sheria ndogo hizi.

“Mfuko wa Elimu” maana yake ni mfuko wa Elimu ulioanzishwa kwenye Halmashauri kwa mujibu wa hseria ndogo hizi.

“Mkuu wa Wilaya” maana yake ni Mkuu wa Wilaya ya Muheza aliyeteuliwa kwa mujibu wa sheria ya Tawala za Mikoa ya mwaka 1997.

“Mkurugenzi” maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza pamoja na Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi.

“Timu ya uendeshaji wa mfuko” maana yake ni Timu ya wataalam inayoshughulikia shughuli za kila siku za mfuko.

“Viwango vya Elimu” maana yake ni viwango vya Elimu ya awali na msingi, Elimu ya sekondari na ufundi vilivyowekwa kwa mujibu wa sera ya Taifa ya Elimu na mafunzo.

“Wadhifa kwenye Chama cha Siasa” maana yake ni kuwa na madaraka ya kuteuliwa au kuchaguliwa kwenye chama chochote cha Siasa kilichoandikishwa chini ya Sheria ya Vyama vya Siasa ya mwaka 1992.

Bodi ya elimu

- 4 (1) Kutakuwa na Bodi itakayojulikana kama Bodi ya Mfuko wa Elimu wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza.
- (2) Bodi itaundwa na wajumbe wafuatao:-
  - (a) Mwenyekiti ambaye atachaguliwa na Mkutano Mkuu wa mwaka wa mfuko kutoka miongoni mwa watu wenye uzoefu na masuala ya Elimu.
  - (b) Katibu Tawala wa Wilaya ya Muheza
  - (c) Wawakilishi wawili watakachaguliwa na Mkutano Mkuu ambapo mmoja kati yao sharti awe mwanamke,
  - (d) Mwakilishi mmoja kutoka miongozi mwa Wakuu wa shule za Shule za sekondari za serikali katika Halmashauri;
  - (e) Mwakilishi mmoja kutoka wamiliki wa shule za binafsi;

- (f) Mwenyekiti wa kamati ya huduma za Jamii wa Baraza la Halmashauri;
  - (g) Wawakilishi wawili kutoka miongoni mwa walimu wakuu wa shule za msingi
  - (h) Mwakilishi mmoja kutoka miongoni mwa makatibu tarafa.
  - (i) Mwakilishi mmoja kutoka wamiliki wa shule za binafsi.
- (3) Bila kuathiri masharti ya kifungu cha 4 (2) cha sheria ndogo hizi Bodi pia itakuwa na wataalamu wafuatao:
- (a) Mkurugenzi mtendaji wa Halmashauri
  - (b) Afisa Elimu wa Halmashauri
  - (c) Mweka Hazina wa Halmashauri
- Ofisi za Bodi 5. Ofisi za Bodi zitakuwa katika eneo la Halmashauri au sehemu nyingine kama bodi itakavyoamua.
- Bodi kualika watu wengine 6. Bodi inaweza kualika watu wengine kwenye vikao vyake kama kutakuwa na haja ya kufanya hivyo lakini hawatakuwa na haki ya kupiga kura.
- Uchaguzi wa mwenyekiti wa Bodi 7. Mwenyekiti wa Bodi atachaguliwa na Mkutano Mkuu wa mwaka wa mfuko baada ya nafasi hiyo kutangazwa katika magazeti yanayosomwa katika eneo la Halmashauri.
- Kipindi cha kushika madaraka 8 (1) Wajumbe wa Bodi watahika madaraka kwa kipindi cha miaka mitatu, lakini mjumbe anaweza kuchaguliwa tena na kuendelea kuwa madarakani kwa kipindi kingine cha miaka mitatu.
- (2) Ufikapo wakati wa uchaguzi wa wajumbe wapya au baada ya kipindi cha muda wa Bodi kuisha, Mkurugenzi Mtendaji atatangaza nafasi wazi na watu wenye sifa hizo watajaza fomu maalum za maombi na kuzirudisha kwenye Halmashauri ndani ya kipindi kitakachowekwa.
- Utaratibu wa kujaza nafasi wazi 9 (1) Pale ambapo nafasi katika Bodi zitakuwa wazi aidha kwa kifo, kujiuzulu, ugonjwa, au kwa sababu nyingine yoyote ile mjumbe mwingine atachaguliwa kujaza nafasi hiyo kwa kipindi kilichobaki.
- (2) Hakuna uchaguzi utakaofanywa endapo kipindi kilichobaki ni cha miezi sita.
- (3) Mjumbe atakayechaguliwa kutokana na sheria ndogo ya 9 (1) hapo juu ataweza kuchaguliwa tena kwa kipindi kingine cha miaka mitatu.

- Uteuzi wa mwisho wa Bodi
- 10 (1) Uteuzi wa wajumbe utathibitishwa na Baraza la Madiwani baada ya kupendekezwa na kamati ya utendaji wa mfuko wa Elimu
- (2) Bodi itazinduliwa rasmi kwa kushuhudiwa na Mkuu wa Wilaya baada ya kuidhinishwa na Baraza la Madiwani.
- kuthibitishwa na Baraza la Madiwani uzinduzi wa Bodi
- 11 (1) Endapo Bodi itazembea kazi au itashindwa kutekeleza kazi zake, Halmashauri itaionya Bodi mara mbili kwa maandishi au kuivunja Bodi na kuandaa uchaguzi mpya ndani ya miezi miwili.
- (2) Endapo Bodi itavunjwa, wajumbe wote wa kuchaguliwa watapoteza nafasi zao na hawatachaguliwa tena kuwa wajumbe wa Bodi ya mfuko wa Elimu.
- (3) Wakati Bodi imevunjwa, Timu ya uendeshaji ya mfuko wa Elimu itatekeleza majukumu ya Bodi hadi hapo Bodi mpya itakapochaguliwa.
- Bodi kuvunjwa kwa kuzembea kazi
- 12 (1) Bodi itafanya vikao vyake vya kawaida kila baada ya miezi mitatu, na vikao vyote vya Bodi vitaendeshwa na mwenyekiti endapo mwenyekiti hatakuwepo, mjumbe mmoja atachaguliwa kutoka miongoni mwa wajumbe kuwa mwenyekiti wa kikao.
- (2) Vikao vya dharura vitafanywa pale tu mwenyekiti atakapoomba au kuombwa kufanya hivyo kwa maandishi na kupata idhini ya wajumbe wasiopungua theluthi moja ya wajumbe wote wanaopiga kura.
- (3) Mjumbe yeyote ambaye bila taarifa au sababu ya msingi atashindwa kuhudhuria vikao vitatu mfululizo vya Bodi atakuwa amepoteza sifa za kuendelea kuwa mjumbe wa Bodi na nafasi yake itatangazwa kuwa wazi.
- Vikao vya bodi
13. Bodi itahakikisha kumbukumbu za Mikutano yake yote zinaandikwa na kuhifadhiwa, pia kumbukumbu za kila Mkutano zitathibitishwa na Bodi kwenye mkutano unaofuata na zitatiwa saini na Mwenyekiti wa Mikutano pamoja na Katibu.
- Kumbukumbu za mikutano ya Bodi
- 14 (1) Nusu ya wajumbe wote ndiyo itakuwa akidi kamili katika vikao vyote vya Bodi.
- (2) Uamuzi wa Bodi utakuwa ni ule unaoungwa mkono wa wajumbe zaidi ya nusu ya wajumbe kamili wa Bodi.
- (3) Wajumbe wa kuchaguliwa wa Bodi ndio watakaokuwa na uwezo wa kupiga kura na kupitisha uamuzi wa Bodi.

- (4) Wataalam na waalikwa hawatakuwa na haki ya kupiga kura.
- (5) Kila mjumbe wa Bodi atakuwa na kura moja na iwapo itatokea kura kufungana mwenyekiti wa Bodi atakuwa na kura ya ziada mbali na kura yake ya kawaida.

Sifa za  
mjumbe wa  
bodi

- 15 (1) Mtu anaweza kushika nafasi ya ujumbe wa Bodi kama atakuwa na sifa zifuatazo:
- (a) Awe raia wa Tanzania.
  - (b) Awe na umri usiopungua miaka ishirini na mitano na asizidi miaka sabini.
  - (c) Awe na akili timamu.
  - (d) Awe na Elimu ya Sekondari, yaani kidato cha nne na kuendelea, isipokuwa endapo hakuna mtu mwenye Elimu ya sekondari basi Halmashauri itatoa idhini kuajiri bila kujali Elimu yake, na
  - (e) Asiwe na madaraka yoyote kwenye chama cha Siasa.
- (2) Mfanyakazi wa Halmashauri hataruhusiwa kuwa mjumbe wa Bodi.

Majukumu na  
kazi za bodi

16. Majukumu na kazi za Bodi zitakuwa kama ifuatavyo:-
- (a) Kubuni mipango na mikakati kwa ajili ya maendeleo ya Elimu katika Halmashauri.
  - (b) Kusimamia mgawanyo wa misaada ya fedha kwa shule kufuatana na Bajeti iliyoidhinishwa na mkutano mkuu wa mwaka wa Bodi.
  - (c) Kusimamia utekelezaji na kutathmini mipango ya Elimu katika Halmashauri;
  - (d) Kujadili na kurekebisha mipango na Bajeti ya Elimu na kuiwasilisha kwenye Mkutano Mkuu wa mwaka wa utendaji kwa ajili ya kuidhinishwa.
  - (e) Kupokea, kuchambua na kuidhinisha Taarifa za utekelezaji wa mfuko wa Elimu wa Halmashauri.
  - (f) Kubuni vyanzo mbalimbali vya mapato na rasilimali za kutosha kuendesha mfuko wa Elimu wa Halmashauri.
  - (g) Kushirikiana na kamati ya huduma za Jamii ya Halmashauri.

- (h) Kuratibu na kusimamia shughuli za maendeleo ya Elimu katika Halmashauri kulingana na programu za kitaifa.
- (i) Kupitisha Kanuni za utekelezaji na utumiaji wa fedha kutoka kwenye mfuko kwa ajili ya kuendeleza madhumuni ya mfuko.
- (j) Kusimamia ujenzi wa shule za sekondari katika Halmashauri.
- (k) Kufanya jambo lolote litakalofanikisha maendeleo ya Elimu katika Halmashauri.

Akidi ya kikao  
na uwezo wa  
kuamua

17. Bodi itakuwa na mamlaka yafuatayo:-

- (a) Kusimamia mgawanyo wa fedha zinazoingizwa kwenye mfuko wa Elimu wa Halmashauri
- (b) Kuajiri na kuachisha kazi watumishi wa Bodi.

Maagizo na  
maelekezo

18. Maagizo, maelekezo, taarifa au hati nyingine zilizotengenezwa au kutolewa kwa niaba ya Bodi zitatiwa saina na:-

- (a) Mwenyekiti wa Bodi, au
- (b) Katibu mtendaji au Afisa mwingine yeyote aliyeidhinishwa kwa maandishi na katibu mtendaji wa Bodi kwa ajili hiyo.

Uhusiano wa  
Bodi na wadau  
na mamlaka  
nyingine.

19. (1) Uhusiano wa Bodi na Jamii, wadau na mamlaka nyingine utakuwa kama ifuatavyo:-

Mamlaka ya  
bodi

- (a) Bodi itahakikisha kuwa jamii inashirikishwa kikamilifu katika kutambua matatizo, kuweka kipaumbele, kupanga, Kuchagua, kufuatilia na kutathmini utoaji wa huduma za Elimu.
- (b) Bodi itawajibika mbele ya Halmashauri ambapo mipango ya Elimu ya robo mwaka na mwaka pamoja na taarifa za kiutaalam za fedha zinapitiwa na kamati ya huduma za jamii na kamati ya fedha, Uongozi na mipango na baadaye kuthibitishwa na Baraza la Halmashauri.
- (c) Bodi itaendesha shughuli zake kwa utaratibu wa uwazi na ambao utakuwa na ufanisi kwa Halmashauri na vyombo vyake vingine vya utendaji bila ya Halmashauri kuingilia uhuru wa Bodi

- (2) Bila ya kuathiri maelezo yaliyomo katika sheria ndogo ya (1) ya sheria ndogo hizi Bodi inaweza kukasimu baadhi ya madaraka yake pale inapoona inafaa.
- Kamati ya huduma za jamii ya Halmashauri
20. Kamati ya huduma za jamii ya Halmashauri itafanya kazi zifuatazo:-
- (1) Itapokea mipango yote ya maendeleo ya mfuko;
  - (2) Itapokea taarifa za ukaguzi wa hesabu za mfuko na kupitia hoja za ukaguzi na baadaye kuziwasilisha kwenye Halmashauri ambayo itaijadili na kuiwasilisha kwa Mkuu wa Wilaya
- Jukumu la Wizara na mamlaka ya Elimu
21. Jukumu la Wizara zinazoshughulikia Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Elimu pamoja na mamlaka ya Elimu itakuwa ni kuandaa Sera, kupanga viwango, kufuatilia na kusimamia shughuli za Bodi kwa mujibu wa sheria zilizopo.
- Katibu mtendaji
22. Bodi kwa idhini ya Mkutano Mkuu wa mwaka, itamteua katibu mtendaji wa mfuko wa Elimu wa Halmashauri.
- Uteuzi wa katibu mtendaji
23. (1) Nafasi ya katibu mtendaji atatangazwa katika magazeti yanayosomwa zaidi nchini atakuwa na sifa zinazofaa.
- (2) Bodi itaamua sifa za watu ambao wataomba nafasi ya katibu mtendaji.
  - (3) Bodi itaamua sifa za watu ambao wataomba nafasi ya katibu mtendaji.
  - (4) Isipokuwa tu kwamba kipindi kimoja cha madaraka kisizidi miaka mitatu na mtu aliyeko madarakani anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kingine cha miaka mitatu.
- Kazi za Katibu mtendaji
24. Kazi za Katibu mtendaji wa Bodi zitakuwa:
- (a) Kuwa mtendaji Mkuu wa shughuli zote za mfuko na katibu wa vikao vyote vya Bodi.
  - (b) Kuongoza, kupanga na kuratibu utendaji wa shughuli za mfuko
  - (c) Kubuni, kuandaa na kusimamia utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya mfuko.
  - (d) Kubuni na kushauri vyanzo mbalimbali vya mapato vya mfuko wa Elimu wa Halmashauri.

- (e) Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya mfuko wa Elimu wa Halmashauri
- (f) Kubuni na kushauri mbinu mbalimbali za kukuza na kuendeleza mfuko wa Elimu wa Halmashauri.

Vyanzo vya mapato ya mfuko

25. Vyanzo vya mapato vya mfuko wa Elimu vitakuwa kama ifuatavyo:- Ruzuku mbalimbali.

- (a) Mchango wa asilimia 2.5 kutoka mapato ya mwaka ya Halmashauri.
- (b) Mchango wa shilingi 2,000/= wa kila mwaka wa kila mwananchi mwenye uwezo wa kufanya kazi anayeishi katika eneo la Halmashauri.
- (c) Misaada mbalimbali kutoka nchi mbalimbali, Taasisi za Kimataifa na Kitaifa, Mashirika ya watu binafsi na Kiserikali, Makampuni binafsi, Madhehebu ya Dini.
- (d) Mikopo.
- (e) Mchango ya mashirika/Makampuni yanayofanya kazi katika eneo la Halmashauri:-
  - (i) Posta 50,000/= kwa mwaka,
  - (ii) Makampuni ya Simu Tshs. 100,000/= hadi 500,000/= kwa mwaka;
  - (iii) Mabenki Tshs. 500,000/= kwa mwaka;
  - (iv) Ranchi Huria Tshs. 200,000/= hadi 500,000/= kwa mwaka
  - (v) Viwanda vya maziwa Tshs. 10,000/= kwa mwaka
  - (vi) Wafanyabiashara wa maduka ya Jumla Tsh. 50,000/= hadi 100,000/= kwa mwaka;
  - (vii) Wafanya biashara wa maduka ya reja reja Tsh. 10,000/= kwa mwaka.
  - (viii) Wafanya biashara wa vituo vya mafuta (Petro filling stations) Tshs. 50,000/= kwa mwaka
  - (ix) Kila kijiji kuchangia Tshs. 100,000/= kwa mwaka.



- (x) Wakandarasi 50,000-100,000/= kwa kazi  
Wazabuni Tsh. 20,000-50,000/= Kwa mwaka
  - (xi) Wadau wengine kama watakavyoibuliwa na kuidhinishwa na halmashauri;
  - (xii) Vyanzo vingine halali vya mapato.
- Fedha za mifuko kulipwa kwenye akaunti
26. Fedha zote zitakazokusanywa, kama fedha za Elimu zitalipwa kwenye akaunti za benki kama bodi itakavyoona inafaa au kuagiza.
27. (1) Kutakuwa na akaunti maalum ya mfuko wa Elimu wa Halmashauri ambapo fedha zote zitawekwa na kutunzwa.
- (2) Wawekaji saine wa akaunti ya mfuko wa Elimu pamoja na taratibu nyingine za mfuko huo zitakuwa kama ilivyoainishwa katika sheria ya mfuko wa Elimu Namba 8 ya mwaka 2001.
- (3) Bodi itaajiri mwaka hazina atakayesimamia akaunti za mfuko wa elimu na kutunza mahesabu yote ya mapato na matumizi.
- Akaunti maalum ya mfuko wa Elimu
28. Fedha zitakazowekwa kwenye mfuko wa Elimu zitatumika kwa madhumuni yakuendeleza, kukuza na kuboresha Elimu kama itakavyokuwa katika mpango wa maendeleo ya Elimu ya Halmashauri.
- Matumizi ya fedha
29. Bodi inaweza kuidhinisha malipo ya fedha kutoka kwenye mfuko kwa madhumuni ya kulipia gharama za:-
- (a) Ujenzi wa shule za sekondari na msingi katika Halmashauri
  - (b) Uendeshaji wa Bodi na kamati ya utendaji.
  - (c) Miradi na programu zinazogharimiwa na mfuko
  - (d) Udhamini wa masomo kwa wanafunzi yatima na wale wasio na uwezo wa kulipia masomo yao.
  - (e) Shughuli nyingine yoyote au zozote ambazo kwa maoni ya Bodi zima manufaa kulingana na malengo na madhumuni ya mfuko.
- Kamati tendaji
- 30 (1) Kutakuwa na kamati ya utendaji ya mfuko wa Elimu wa Bodi.
- (2) Kamati Tendaji itakuwa na wajumbe wafuatao:-
- (a) Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ambaye atakuwa Mwenyekiti,

- (b) Katibu mtendaji wa Bodi ambaye atakuwa katibu,
- (c) Afisa Elimu Msingi wa Halmashauri ambaye atakuwa mjumbe,
- (d) Afisa Elimu Msingi wa Halmashauri ambaye atakuwa mjumbe,
- (e) Mweka hazina wa Bodi ambaye atakuwa mjumbe,
- (f) Mchumi wa Halmashauri ambaye atakuwa mjumbe.

31. Kazi za kamati tendaji zitakuwa kama ifuatavyo:-

- (a) Kuandaa taarifa za utekelezaji za mfuko wa Elimu na maendeleo ya Elimu katika Halmashauri
- (b) Kuandaa mipango kabambe ya Elimu ya Halmashauri ambayo itatilia mkazo mahitaji ya Elimu ya Halmashauri kwa kuzingatia mwongozo wa kitaifa wa mpango wa Elimu
- (c) Kuwezesha na kuratibu vikao vya Bodi ya mfuko wa Elimu pamoja na mkutano mkuu wa mwaka.
- (d) Kuchambua na kubainisha maeneo ya kipaumbele kwa masuala ya Elimu katika Halmashauri.
- (e) Kuweka taratibu na vigezo vya ufadhili wa wanafunzi na utoaji ruzuku kwa miradi ya Elimu katika Halmashauri.
- (f) Kuweka taratibu na vigezo vya ufadhili wa wanafunzi na utoaji ruzuku kwa miradi ya Elimu katika Halmashauri.

Mkutano mkuu  
wa mwaka wa  
mfuko

32. Kutakuwa na Mkutano Mkuu wa mwaka wa mfuko wa Elimu utakaokuwa na wajumbe wafuatao:

- (a) Wajumbe wote wa Bodi ya mfuko wa Elimu
- (b) Kamati tendaji ya mfuko wa Elimu
- (c) Wawakilishi toka madhehebu ya Dini.
- (d) Wajumbe wa kamati ya huduma za jamii.

Majukumu ya  
Mkutano  
Mkuu

33. Bila kuathiri uwezo wa Bodi, Mkutano Mkuu wa mwaka kitakuwa ndicho chombo cha:-

- (a) Kupokea tarifa za ukaguzi wa mahesabu na utendaji wa mfuko za mwaka.
- (b) Kumteua mwenyekiti wa Bodi na wakaguzi wa hesabu za mfuko.

- (c) Kuchagua wawakilishi wawili wa bodi kutoka miongoni mwa wadau wa Elimu
- Taarifa ya mapato na matumizi 34. Katibu mtendaji atatarisha na kuwasilisha kwenye Bodi kila baada ya miezi mitatu taarifa iliyo na:-
- (a) Viashiria vya utendaji na taarifa nyingine zinazohusiana na shughuli za bodi.
- (b) Kazi zilizofanyika na mafanikio yaliyopatikana
- (c) Taarifa nyingine kwa kadri Bodi itakavyoona inafaa.
- Sheria Na. 33 ya mwaka 1972 35. (1) Katibu mtendaji atatumza hesabu na kumbukumbu za shughuli zake, na atahakikisha kuwa fedha zote zilizopokelewa zinaingizwa kwenye akaunti na kwamba malipo yote kutoka kwenye mfuko yanafanywa kwa usahihi baada ya kuidhinishwa na ataweka udhibiti wa kutosha wa mali zake pamoja na madeni.
- (2) Hesabu za mwaka za mfuko wa Elimu wa Halmashauri zitakaguliwa na Mkaguzi na mtaalamu mwenye sifa ya Ukaguzi aliyesajiliwa chini ya Sheria ya usajili wa Wahasibu na Wakaguzi ya mwaka 1972 na ambaye ameteuliwa na Mkutano Mkuu.
- (3) Ndani ya kipindi cha miezi sita baada ya mwisho wa kila mwaka wa fedha Bodi itatarisha na kuwasilisha kwa Halmashauri taarifa ya fedha ya mwaka huo ambayo itajumuisha:-
- (a) Taarifa za fedha,
- (b) Viashiria vya utendaji na taarifa nyingine zinazohusiana nazo
- (c) Taarifa ya utekelezaji ya mfuko wa Elimu wa Halmashauri.
- Mkuu wa Wilaya kuwasilisha taarifa ya mwaka 36. Mkuu wa Wilaya atawasilisha nakala ya taarifa ya kila mwaka kwenye Mkutano Mkuu wa mwaka wa mfuko.
- Bodi kuwa na uwezo wa kukagua 37. Bodi itakuwa na madaraka ya kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa hesabu za mfuko wa Elimu.
- Makosa na Adhabu 38. Mtu yeyote ambaye:-
- (a) Atakwenda kinyume na masharti ya sheria ndogo hizi au;

- (b) Atakayefanya kitendo chochote ambacho kitazuia Bodi au kamati tendaji kufanya kazi zake kwa ufanisi au;
  - (c) Atatumia vibaya mali na rasilimali za mfuko wa Elimu na kusababisha kutofikiwa kwa malengo yaliyowekwa, au;
  - (d) Kwa uzembe atashindwa kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa sheria ndogo hizi;
  - (e) Kwa namana yoyote ile atashawishi watu wasitelekeze lolote chini ya sheria ndogo hizi.
- Atakuwa ametenda kosa la jinai na akipatikana na hatia atalipa faini isiyozidi shilingi mia tatu elfu (300,000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote faini na kifungo kwa pamoja.

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Muheza ilibandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa kufuata azimio lililopitishwa kwenye mkutano wa Halmashauri uliofanyika mnamo tarehe 31 mwezi wa 10 Mwaka 2012 na nembo hiyo ilibandikwa mbele ya:

Ibrahim M. Matovu  
MKURUGENZI MTENDAJI HALMASHAURI YA  
WILAYA YA MUHEZA

Amir Abdulrahman Kiroboto  
MWENYEKITI WA HALMASHAURI YA WILAYA  
MUHEZA

Nakubali

Mhe. MIZENGO P. PINDA  
WAZIRI MKUU

DODOMA.

Tarehe.....